

# Pata faida halal na



## Sukuk

Hili ni neno la Kiarabu linalomaanisha hati fungani za Kiislamu au vyeti vya kifedha vinavyokubaliana na misingi ya Sharia.

## Sukuk na Hati Fungani za Kawaida

Sukuk zinatofautiana na hati fungani za kawaida (bonds) kwa muundo na uhalali wa kisheria wa Kiislamu. Wakati hati fungani zinawakilisha deni na si halali kisheria Kiislamu kwa sababu zinategemea riba, Sukuk zinaundwa kwa kuzingatia kanuni za Kiislamu na zinawakilisha umiliki wa sehemu ya mali msingi.

Tofauti na hati fungani, ambazo mara nyigi hazina dhamana na zinategemea tu uaminifu wa mkopeshaji, Sukuk mara nyigi zinatokana na mali halisi au mali zenydhamana. Mapato kutoka Sukuk hutokana na faida au mapato yanayozalishwa na mali hizo, badala ya malipo ya riba, na hivyo kufuata kikamilifu misingi ya fedha za Kiislamu.

## Kuhusu CRDB Al-Barakah

CRDB Al-Barakah inatoa huduma za kifedha zinazokubaliana na Sharia kwa wateja wanaopendelea huduma za kibenki za maadili, zisizo na riba, na zinazofuata kanuni za Kiislamu.

## CRDB Al-Barakah Sukuk

CRDB Al-Barakah Sukuk inamalengo ya uwekezaji wenye uwajibikaji wa kijamii. Sukuk hii inatokana na muundo wa ijarah (kodi ya mali) unaokubaliana na Sharia pia mtu yoyote anaweza kununua SUKUK hii, sio lazima mtu mwenye imani ya Kiislamu, inawakaribisha wote.

Inawapa wawekezaji mapato yenye hatari ndogo na yenye kiwango cha mapato kilichowekwa, huku ikikuza ufadhili wa kimaadili na unaoendana na Sharia.

## MAELEZO YA UTOAJI WA SUKUK

<b>Mtoaji:</b>	CRDB Bank Plc kupitia Al Barakah Banking
<b>Muundo wa Sukuk:</b>	Ijarah (Makubaliano ya upangishaji mali)
<b>Kiasi cha Utoaji:</b>	<ul style="list-style-type: none"><li>TZS 30,000,000,000</li><li>USD 5,000,000</li></ul>
<b>Muda wa Uwekezaji:</b>	Miaka 5
<b>Kiwango cha Faida kwa Mwaka:</b>	<ul style="list-style-type: none"><li>TZS: 12% kwa mwaka</li><li>USD: 6% kwa mwaka</li></ul>
<b>Tarehe ya Kufungua Ofa:</b>	9 Agosti 2025
<b>Tarehe ya Kufunga Ofa:</b>	12 Septemba 2025
<b>Tarehe ya Kutoa Sukuk:</b>	8 Oktoba 2025
<b>Tarehe ya Kukomaa kwa Sukuk:</b>	8 Oktoba 2030
<b>Tarehe za Malipo ya Faida:</b>	8 Januari, 8 Aprili, 8 Julai, 8 Oktoba ya kila mwaka

## Matumizi ya Mapato

Mapato yatakayopatikana kutokana na mauzo ya Sukuk yatatumika kufadhili ukuaji na upanuzi wa shughuli za CRDB Al Barakah, pamoja na uwezeshaji kwa biashara na miradi inayozingatia misingi ya Sharia. Aidha, fedha hizi zitaelekezwa kwenye upanuzi wa bidhaa mbalimbali za kifedha za Kiislamu zinazoweza kutolewa na CRDB Al Barakah.

## **Wawekezaji Wanaostahiki Sehemu ya TZS (Shilingi za Kitanzania)**


Wawekezaji binafsi (wa ndani ya nchi, walioko ughaibuni, na wageni)  
Vikundi vya uwekezaji  
Uwekezaji wa pamoja (mfano: wanandoa)  
Makampuni binafsi na ya Serikali

### **Sehemu ya Dola za Kimarekani (USD)**

Wawekezaji binafsi (wa ndani ya nchi, walioko ughaibuni, na wageni)  
Vikundi vya uwekezaji  
Uwekezaji wa pamoja (mfano: wanandoa)  
Makampuni binafsi na ya Serikali

### **Jinsi ya Kuwekeza**

Pakua au ingia kwenye SimBanking App ya CRDB ili kuwekeza kwa urahisi, popote ulipo.




Fungua SimBanking App  
kwenye simu yako  
(pakua kutoka Play Store au  
App Store kama bado huna).

**Ingia kwa kutumia:**  
Namba yako ya simu au jina  
la mtumiaji (username)

Nenosiri lako au PIN

Katika menu kuu, **gonga  
sehemu ya "Miniapps"**

3



Chagua  
Investmen/Uwekezaji

4




Chagua  
“AI Barakah Sukuk”

5




Chagua  
“Invest Now/wekeza”

6




Weka kiasi cha pesa ya  
kitanzania au Dola unataka  
kuwekeze kisha bonyeza  
“Endelea”

**7**

Ikiwa unayo, weka namba yako ya CDS (Central Depository System), na kama hauna bonyeza sina, itakutengenezea namba yako ya CDS (Central Depository System)

**8**


Hakiki taarifa zako

**9**

Chagua akaunti unayotaka kulipia uwekezajo yako kisha bonyeza “**Endelea**”

**10**

Utapokea namba ya kumbukumbu ya kulipia kisha bonyeza “**Lipa Sasa**”



Utapokea risit ya malipo,  
itunze kwa ajili ya rekodi zako

Kwa maelezo au maswali ya ziada tafadhali wasiliana na sisi kupitia;

Barua Pepe: info@crdbbank.co.tz  
Namba ya simu: +255(22)2197700 | +255(0)714197700  
+255(0)755197700 | 0800008000

